# JUMUIYA YA KIKRISTO TANZANIA (CCT)

# TANGAZO LA KAZI

**UTANGULIZI;**

Jumuiya ya Kikristo Tanzania ambayo inajulikana kwa kifupi kama CCT (Christian Council of Tanzania), ni Taasisi ya Ki-ekumene inayowakilisha Umoja wa Madhehebu ya Kikristo ya Kiprotestanti. Jumuiya ya Kikristo Tanzania ilianzishwa mwaka 1934 na rasmi mwaka 1955 ilianza kutambulika kwa jina la Jumuiya ya Kikristo Tanganyika, na baada ya muungano wa Tanganyika na Zanzibari jina lilibadilika rasmi na kuitwa Jumuiya ya Kikristo Tanzania mnamo mwaka 1965.

Idadi ya Makanisa yaliyopo chini ya CCT imekuwa ikiongezeka kutoka Makanisa matatu (3) ya mwanzo hadi kufikia Makanisa ya Kiprotestanti kumi na mbili (12) ambayo ni; Kanisa la Moravian Tanzania (MCT), Kanisa la Anglikana Tanzania, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Kanisa la Afrika Inland Tanzania (AICT), Kanisa la Mennonite Tanzania (KMT), Kanisa la Uinjilisti Tanzania, Kanisa la Upendo wa Yesu Kristo Masihi (KIUMA), Kanisa la Mungu Tanzania, Kanisa la Biblia Tanzania, Kanisa la Jeshi la Wokovu Tanzania, Kanisa la Presbyterian la Afrika ya Mashariki na Kanisa la Wabaptisti Tanzania.

Hivyo basi, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania anakaribisha maombi ya kazi ili kuweza kujaza nafasi kama ifuatavyo;

1. **MKURUGENZI WA UTUME NA UINJILISTI - NAFASI 1**

**Msimamizi:** Katibu Mkuu

**Kituo cha Kazi:** CCT –Makao Makuu Dodoma

**Muda wa Mkataba:** Miaka 3 (Unaweza Ongezeka)

## Kurugenzi ya Utume na Uinjilisti – CCT

Kurugenzi ya Utume na Uinjilisti inafanya kazi ya kuratibu Shughuli zote za utume na Uinjilisti ndani ya CCT kupitia makanisa wanachama ya CCT. Shughuli hizo ni pamoja na: kuratibu mafundisho ya Elimu ya Kikristo shule za awali, shule za msingi, Sekondari, malezi ya wanafunzi kupitia UKWATA katika shule za Sekondari na USCF katika vyuo vya kati na vyuo vikuu. Kurugenzi inaratibu Makanisa ya Vyuo vikuu yaani Chaplaincies nchini, Kuratibu uundwaji wa Kamati za Vijana, Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na Uongozi wa CCT Mikoani. Kurugenzi inaratibu pia shughuli zote za Ki-ekumene kulileta Kanisa katika Umoja na Ushirikianao kama Wakristo. Zaidi ya hayo, Kurugenzi inaratibu shughuli za Mahusiano ya Dini Mbalimbali (Interfaith Relations) ambapo inasimamia uundwaji wa Kamati za Dini Mbalimbali katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Kata kwa kushirikiana na Baraza kuu la waislamu wa Tanzania (BAKWATA), Baraza la Maaskofu wa katoliki Tanzania (TEC), Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya kipentekoste Tanzania (CPCT) na Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA) kwa lengo la kudumisha Mahusiano mema baina ya viongozi wa Imani tofauti kwa ajili ya Amani ya Nchi yetu.

### A. Majukumu Ya Mkurugenzi wa Utume na Uinjilisti – CCT

1. Kuratibu na kusimamia shughuli za Utume na Uinjilisti ndani ya CCT kwa kushirikiana na Makanisa na vyama wanachama.
2. Kuandaa na kusimamia vikao vya Chaplaincies za CCT na Mkutano mkuu wa mwaka wa Chaplaincies zote.
3. Kusimamia uratibu wa Mikutano mikuu ya kitaifa ya UKWATA na USCF
4. Kuandaa bajeti ya Kurugenzi, mapato na matumizi
5. Kuandaa Taarifa ya Kazi itakayowasilishwa kwenye vikao vya Menejimenti ya Wakurugenzi CCT
6. Kuandaa na kusambaza (Mitaala) machapisho mbalimbali ya Elimu ya Kikristo, UKWATA, USCF na Chaplaincies
7. Kuandaa Mitihani ya Elimu ya Kikristo, kwa wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari wanaotoka katika Makanisa wanachama wa CCT.
8. Kuandaa Semina na Mikutano ya Ki-ekumene Kitaifa na Kimataifa.
9. Kushiriki Warsha/ Mikutano mbalimbali kwa taratibu za Taasisi
10. Kuratibu dawati la Mahusiano ya Dini mbalimbali na kuongoza Majadiliano mema ya Kidini (interfaith dialogue)
11. Kuandaa makisio ya dawati, ripoti na kuwasilisha kwa wadau husika
12. Kuratibu na kusimamia Makanisa ya vyuo vikuu
13. Kusimamia Wachungaji wa Makanisa ya vyuo vikuu.
14. Kuandaa mipango na bajeti ya Kurugenzi ya Utume na Uinjilisti
15. Kuandaa na kuweka mikakati ya Uinjilisti wa pamoja kwa kushirikiana na Makanisa wanachama katika ngazi za mikoa.
16. Kufanya kazi zingine zozote zitakazopangwa na taasisi.

## B. Sifa za Mkurugenzi wa Utume na Uinjilisti - CCT

i. Awe Mchungaji kutoka Makanisa Wanachama wa CCT
ii. Awe na Shahada ya kwanza ya Theolojia kutoka chuo kinachotambulika.
iii. Awe na Elimu ya shahada ya Uzamili au zaidi kutoka chuo kinachotambulika.
iv. Awe na uzoefu wa utumishi katika Kanisa/taasisi za dini usiopungua miaka mitano.
v. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania, wenye umri kuanzia miaka 35 na usiozidi miaka 50.
vi. Awe ni Mchungaji mwaminifu, mwadilifu na mwenye ushuhuda mzuri kutoka Kanisa mwanachama wa CCT.
vii. Awe na uwezo wa kuongoza na kushirikisha wengine katika kazi na majukumu yake.
viii. Awe na ufahamu wa kutosha juu ya mifumo ya Kanisa ndani na nje ya Kanisa lake
ix. Awe na uzoefu wa kushirikiana na vijana (UKWATA na USCF).
x. Awe tayari kusafiri kikazi pindi atakapohitajika.
xi. Awe na uwezo mzuri wa kutumia kompyuta.
xii. Awe na ujuzi wa udereva.

## C. Viambatanisho vya lazima kwa waombaji wote

i. Barua ya maombi
ii. Cheti cha kuzaliwa
iii. Maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika.
iv. Barua (recommendation letter) kutoka kwa Mkuu wa Kanisa analotoka.
v. Majina ya wadhamini watatu (referees) wa kuaminika, anuani na namba za simu.
vi. Nakala ya vyeti vya taaluma na uzoefu
vii. Leseni ya udereva.

## D. Jinsi ya kutuma Maombi:

i. Maombi yote yatumwe kwa
Katibu Mkuu,
Jumuiya ya Kikristo Tanzania,
S.L.P 1454
DODOMA,

Christian Council of Tanzania
P.O. Box 1454 - Dodoma
Tanzania

ii. Maombi yote (scanned pdf file moja) yatumwe kupitia barua pepe tu;

***recruitment@cct.or.tz***

iii. Maombi ya kutumwa kwa mkono au posta hayatapokelewa.

iv. Mwisho wa kutuma maombi ni **Tarehe 26/09/2025, saa 10:00 Jioni.**

v. Watakaochaguliwa kwa ajili ya hatua ya usaili watajulishwa.